## Ufafanuzi wa Mada

# Haki ya Kujieleza

Muhtasari uliofanywa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

## Ujumbe Muhimu:

***Haki ya uhuru wakujieleza ni shaki ya msingi ndani ya taifa la kidemokrasia. Haki hii inalindwa kikatiba lakini inaminywa kivitendo kupitia sheria mbalimbali. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapendekeza kutungwa kwa sheria itakayohakikisha Uhuru wa Kujieleza unapata ulinzi madhubuti kama inavyolindwa na Katiba ya nchi.***

Haki ya Uhuru wa Kujieleza ni haki inayolindwa kikatiba ijapokuwa bado inaminywa. Haki ya uhuru wa kujieleza inahusisha haki ya kutafuta, kupokea na kusambaza taarifa na mawazo. Haki hii ina uwanda mpana. Kwa kuangalia dhana ya kusambaza taarifa na mawazo, haki hii inahusisha haki ya mtu kujieleza ana kwa ana, kwa maandishi au kwa kutumia njia nyingine za mawasiliano pamoja na njia za kielektroniki.

Haki ya uhuru wa kujieleza inahusisha pia haki ya kutafuta na kupokea taarifa kutoka kwa wengine, pamoja na haki ya kupata na kusoma magazeti, kusikiliza matangazo, kutumia mtandao wa intaneti na kuhusika na kushiriki kwenye mijadala ya umma au binafsi.

Haki ya Uhuru wa Kujieleza inalindwa na Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, chini ya Ibara ya 18. Haki hii pia inalindwa na mikataba mbalimbali ya kimataifa kama vile Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu katika Ibara ya 19, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kisiasa na Kiraia katika Ibara ya 19, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu katika Ibara ya 9.

Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kisiasa na Kiraia umeorodhesha masharti kadhaa ambayo yanapaswa kufuatwa wakati wa kutafuta, kupokea na kusambaza taarifa. Hii ina maana kuwa Haki ya Uhuru wa Kujieleza inaweza kuwekewa mipaka ya utekelezwaji wake na Dola, isipokuwa tu mipaka hiyo lazima iwe na viwango vifuatavyo:

1. Mipaka inayowekwa inawekwa kwa mujibu wa sheria au kanuni;
2. Mipaka iliyowekwa kisheria lazima iwe inalinda na kukuza lengo halali lililowekwa na sheria za kimataifa;[1] na
3. Mipaka hiyo lazima iwe ya lazima kwa ajili ya ulinzi au kukuza lengo halali: Matokeo ya mipaka hii lazima iwe ya uwiano – madhara/mipaka ya Haki ya Uhuru wa Kujieleza lazima isizidi faida ya maslahi iliyokusudiwa.

Hivyo basi, ni muhimu kuhakikisha kuwa mipaka yoyote itakayowekwa katika utekelezaji wa Haki ya Uhuru wa Kujieleza, inafuata masharti yaliyowekwa na mikataba ya kimataifa kama ilivyoainishwa hapo juu.

## Mambo ya Kuzingatia:

Kuna mambo kadhaa muhimu ya kutatua ili kuhakikisha kuwa Haki ya Uhuru wa Kujieleza inazingatiwa na kulindwa kwa ajili ya wananchi wa Tanzania.

### 1. Kukosekana kwa Sheria Zinazolinda Haki ya Uhuru wa Kujieleza kama ilivyo katika Katiba:

Taarifa ya Haki za Binadamu ya Mwaka 2015 inayotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ilionyesha kuwa, 'Licha ya kuwa na ulinzi wa kikatiba, kwa sasa hakuna sheria nchini Tanzania ambayo inasimamia ulinzi huu wa kikatiba wa Haki ya Uhuru wa Kujieleza.' Uwepo wa sheria ni kiungo muhimu sana cha kuwa na ulinzi madhubuti wa Haki ya Uhuru wa Kujieleza. Kama hiyo haitoshi, vilevile hakuna sheria ambayo inahakikisha kuwepo kwa ulinzi wa maeneo mengine ya haki hii. Sheria inahitajika ili kuweka dhima na wajibu wa Dola na raia, na kuweka miundombinu inayohitajika kuweka mwongozo wa namna ya kushughulikia ukiukwaji wa haki hii. Juhudi za kutunga sheria ya kulinda haki hii zimekwama kwa muda mrefu tangu mwaka 2006. Kama ilivyoonyeshwa na Taarifa ya Haki za Bnadamu ya mwaka 2015, mchakato wa kurekebisha Katiba ilikuwa fursa nzuri ya kuhakikisha kuwa kasoro za kikatiba na kisheria zinarekebishwa, lakini kwa bahati mbaya mchakato wa marekebisho ya Katiba umesimama. Kukosekana kwa sheria hii kunamaanisha kuwa Haki ya Uhuru wa Kujieleza inakosa ulinzi thabiti.

1. Hii inahusisha malengo halali yafuatayo: (1) heshima kwa haki na sifa za wengine, au (2) ulinzi wa Usalama wa Taifa, Utaratibu wa Umma, afya ya jamii na maadili.

Kama ilivyoonyeshwa na Taarifa ya Haki za Bnadamu ya mwaka 2015, mchakato wa kurekebisha Katiba ilikuwa fursa nzuri ya kuhakikisha kuwa kasoro za kikatiba na kisheria zinarekebishwa, lakini kwa bahati mbaya mchakato wa marekebisho ya Katiba umesimama. Kukosekana kwa sheria hii kunamaanisha kuwa Haki ya Uhuru wa Kujieleza inakosa ulinzi thabiti.

## 2. Uwepo wa Sheria Nyingi Zinazobana Uhuru wa Kujieleza:

Kwa upande mwingine, Tanzania ina sheria nyingi zinazoonekana kwa namna moja au nyiingine kubana Uhuru wa Kujieleza nchini. Miongoni mwa sheria hizi ni Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976, Sheria ya Magazeti ya Zanzibar ya mwaka 1976, Sheria ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1970, Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma za mwaka 1995, Sheria ya Utangazaji Tanzania ya mwaka 1993, Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002, Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ya mwaka 2003 na sheria nyingine za hivi karibuni kama Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ya mwaka 2015 na Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015.

Taarifa ya Haki za Binadamu ya mwaka 2015 inatoa uchambuzi wa kila mojawapo ya sheria hizi. Sheria hizi zinatoa upendeleo kwa serikali na mamlaka zake bila kujali maslahi mapana ya jamii. Sheria hizi zinakiuka Haki ya Uhuru wa Kujieleza kama ulivyowekwa na Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Tanzania ya mwaka 1977. Nyingi ya sheria hizi zimepitwa na wakati na zimetungwa wakati kukiwa na muktadha tofauti wa kisiasa na kiuhalisia. Tasnia ya habari imebadilika sana nchini kwa kipindi cha muongo mmoja uliopita, ambapo tumeshuhudia kukua kwa mawasiliano kwa njia ya mtandao wa komputa, simu za mikononi na teknolojia ya mitandao ya kijamii. Kuna haja ya kuangalia umuhimu wa njia hizi mpya za upashanaji habari wakati tunapoendelea na mchakato wa Marekebisho ya Katiba.

## 3. Sheria ya Makosa ya Mtandaoni imeleta uwoga kwa watu wanaotumia mitandao ya kijamii na mawasiliano ya intaneti kwa ajili ya shughuli za uangalizi na utetezi:

Sio tu kwamba Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ya mwaka 2015 inaweka vikwazo kwenye Haki ya Uhuru wa Kujieleza lakini pia inaweka vikwazo kwenye maendeleo. Kuharamishwa kwa shughuli zinazofanywa mtandaoni kunatengeneza uwoga kwa watu wanaojihusisha na shughuli za uangalizi na utetezi wa masuala ya haki za binadamu.

Sheria hii pia haizingatii haki ya kikatiba ya kutafuta, kupokea na kuchapisha taarifa. Ni Dhahiri kuwa sheria hii ina maudhui mazuri ya kuhakikisha kuwa kunakuwa na utaratibu wa kushughulikia masuala ya kimitandao, hasa katika kuzuia shughuli haramu zinazofanywa kupitia mitandao. Hata hivyo, Sheria ya Makosa imeweka mkazo zaidi katika kuharamisha shughuli zinazofanyika mtandaoni na kutokutilia mkazo katika kushughulikia masuala ya kimtandao ambayo ni halali. Taarifa ya Haki za Binadamu ya mwaka 2015 ilionyesha kuwa, 'sheria hii pia inavifungu kadhaa ambavyo ni tata na vyenye ubishani kuhusiana na kuharamishwa kwa kubadilishana kwa taarifa, nguvu maradufu walizopewa polisi za kupekua na kupokonya, kufanya uchunguzi bila kuwa na amri halali ya mahakama pamoja na tafsiri nyingine tata za makosa mbalimbali.' Kuna hatari kuwa sheria hii itaathiri sana utendaji wa Taasisi zisizo za Kiserikali katika matumizi ya Teknolojia kama vile simu za mikononi katika kazi za utetezi na uangalizi wa shughuli za serikali.[2]

Mtandao wa Web Index ambao ni kielezo cha kimataifa, kipo kwa ajili ya kupima uzito wa namna gani raia wa nchi wanaweza kufurahia haki ya habari, mawazo, kujieleza, usalama na faragha mtandaoni. Mwaka 2014 Tanzania iliwekwa katika nafasi ya 67 miongoni mwa nchi 86 katika masuala yanayohusiana na uhuru wa kujieleza na uwazi katika masuala ya upatikanaji wa mtandao wa intaneti, ambayo inaonyesha kuwa imebanwa zaidi kwa kulinganisha na nchi za Uganda, Kenya na Nigeria.[3]

2. Kwa taarifa Zaidi na uchambuzi wa Sheria hii tafadhali angalia uchambuzi uliofanywa na Ushirikiano wa Sera ya Kimataifa ya Teknolojia ya Ha bari na Mawasiliano (ICT) kwa upande wa Afrika Masshariki na Kusini (CIPESA).

3. Tafadhali tembelea http://thewebindex.org/about/kwa taarifa zaidi juu ya Kielezo hichi na takwimu zaidi.

Zoezi hili lilifanyika kabla ya kupitishwa kwa Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ya mwaka 2015, na Sheria ya Mawasiliano ya Kieletrooniki na Posta, sheria ambazo zinaweza kwa kiasi kikubwa kuathiri nafasi ya Tanzania katika kielezo hiki.

## 4. Kuminywa kwa Uhuru wa vyombo vya habari:

Mojawapo ya vitu muhimu vinavyoathiri Haki ya Uhuru wa Kujieleza ni uhuru wa vyombo vya habari. Nchini Tanzania ubora wa utoaji wa taarifa wa vyombo vya habari umekuwa unafanyiwa uchunguzi sana, taarifa zinazotolewa kihisia zinaweza kuwa na athari kwa mawazo ya raia juu ya kuaminika kwa namna ya utoaji taarifa wa vyombo vya habari. Mwaka 2014, *Afrobarometer* - ambayo inafanya upimaji kwa jamii juu ya demokrasia na utawala barani Afrika – ilionyesha kuwa na ongezeko la raia nchini Tanzania ambao wanadhani kuwa serikali inatakiwa idhibiti maudhui ya machapisho ya vyombo vya habari, ukilinganisha na miaka miwili iliyopita (asilimia 26 mwaka 2012 na asilimia 44 mwaka 2014).

Mwendelezo huu unatia shaka. Kuna hatari kuwa takwimu hizi zinaweza kutumiwa kuhalalisha kusudi la kisiasa kwa ajili ya kuzidisha kubanwa kwa uhuru wa vyombo vya habari. Badala yake, nguvu zaidi inatakiwa kuelekezwa katika kuboresha ubora wa taarifa za vyombo vya habari na kuimarisha mawazo ya raia juu ya umuhimu wa kuwa na vyombo huru vya habari.

Zaidi ya hayo, kama ilivyoelezwa mwanzoni, kumekuwepo na sheria zilizo na athari kwa vyombo vya habari. Taarifa ya Haki za Binadamu ya mwaka 2015 inaonyesha kuwa gazeti la *the East African* lilifungiwa na serikali hapo Januari 2015 chini ya kifungu cha 6 cha sheria ya Magazeti ya mwaka 1976. Kufungiwa kwa gazeti hili kunafuatia muendelezo wa gazeti hili kuandika Makala mbalimbali ambazo zilikuwa zinakosoa serikali.

## 5. Sheria ya Takwimu inaminya ukusanyaji, utumiaji na usambazaji wa takwimu huru:

Taarifa ya Haki za Binadamu ya mwaka 2015 masuala mbalimbali dhidi ya Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015. Masuala hayo ni kama:

(a) inaweka mazingira yasiyokuwa ya uhakika juu ya nani anaweza kutengeneza takwimu na nani anatakiwa kuidhinisha,
(b) kanuni juu ya usambazaji wa takwimu,
(c) vikwazo kwa watoa taarifa bila kuwalinda, na
(d) masharti juu ya uchapishaji wa mawasiliano kuhusu masuala bishani/shindani.5 Kuna wasiwasi kuwa Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015 inaweza kutumika kama silaha ya kisiasa kwa ajili ya kuchuja takwimu ambazo haziipendezi serikali. Sheria hii inaweza pia kuminya tafiti zinazofanywa na asasi za kiraia na watafiti huru.

## 6. Upatikanaji wa taarifa bado unaminywa pamoja na juhudi za kuweka taarifa za umma wazi zaidi

Serikali imefanya juhudi za makusudi kuhakikisha taarifa za umma zinapatikana kwa urahisi. Hata hivyo, taarifa hizi hazirekebishwi mara kwa mara kuweka taarifa mpya na kunakuwa na ugumu wa kuzipata taarifa hizi. Ushirikiano juu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa nchi za Afrika Mashariki na Kusini (CIPESA) ulitoa taarifa juu ya upatikanaji wa taarifa na kugundua kuwa taarifa hizi hazirekebishwi mara kwa mara na kwa kuweka taarifa mpya; zipo katika mfumo ambao taarifa haziwezi kufanyiwa kazi kwa mfumo mwingine na mara nyingi taarifa hizi hazikidhi viwango vya lugha husika.

4. Tafadhali angalia ukurasa wa 62

# Fursa na Ujumbe Muhimu

## 1. Utungaji wa sheria zinazoathiri Haki ya Uhuru wa Kujieleza uangaliwe upya kwa kuhusisha wadau mbalimbali

Ili Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (ambayo inaongelea juu ya Haki ya Uhuru wa Kujieleza) iwe na maana kuna ulazima basi wa kutunga sheria ambayo itahakikisha utekelezwaji na ulinzi wa haki hii. Sheria zinatakiwa kuweka bayana haki, jukumu na wajibu wa ulinzi wa Haki ya Uhuru wa Kujieleza kwa serikali na raia. Hii haihitaji kuanzia mwanzo kabisa kwa sababu miswada ya sheria imekwisha andaliwa; Hata hivyo, miswada hii inatakiwa iangaliwe upya na kurekebishwa kwa kuwahusisha wadau na katika hali ya ushirikishi ili kuhakikisha kuwa miswada hii inakuwa na muktadha wa wakati husika.

Mchakato wa kutunga sheria mpya ulianzishwa miaka ya 2000 na Umoja wa Asasi za kiraia. Ikiwa kama sehemu ya mchakato huu, Umoja huu ulitengeneza rasimu ya sheria mbalimbali zikiwemo Mswada wa Sheria ya Upatikanaji habari. Serikali ilichukua baadhi ya maudhui ya mswada huu lakini wakati wa kutunga sheria masuala mbalimbali yaliyokuwa katika muswada yakatupiliwa mbali. Mnamo mwaka 2015 Mswada wa Upatikanaji Habari ulipelekwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na sheria kupitishwa. Hata hivyo, mchakato mzima na mswada ulikosolewa sana na wadau. Maoni ya wadau wa habari na asasi za kiraia yanaonekana kuwa hayakuzingatiwa wakati wa mchakato.

Miongoni wa maoni ya wadau hao ilikuwa ni kuwa na chombo huru cha usimamizi wa habari lakini mswada haukuzingatia haya. Muhimili wa Serikali ulipewa nguvu kubwa za kimahakama. Mwisho wa siku mswada huu ukashindwa kupitishwa. Kwa kuangalia uwezo na changamoto za mchakato mzima, kuna fursa ya kurudiwa tena na kuhakikisha kuwa wadau wanahusishwa ipasavyo.
Sheria hazitakiwi kupitishwa kwa njia ya 'hati ya dharura' ambayo inaipa uwezo serikali kuharakisha mchakato mzima, kama ilivyofanyika kwa Mswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Habari. Njia hii haitoi nafasi ya kutosha kwa asasi za kiraia na wadau wengine kupitia vizuri mchakato mzima. Tunapendekeza kuwepo na mchakato shirikishi ambao utaongozwa na Baraza la Habari Tanzania kwa usaidizi wa kisheria kwa asasi kama Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

## 2. Vifungu vya sheria vibadilishwe na baadhi ya sheria zifutwe:

Kama mswada mpya wa Uhuru wa Kujieleza utapitishwa na kutungwa kuwa sheria basi sheria hiyo lazima iwe na vifungu ambavyo vitafuta vifungu vya sheria zilizopo ambavyo vinavunja Haki ya Uhuru wa Kujieleza. Tunapendekeza pia kuwa Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 ifutwe kabisa kwani ni ya kale na kandamizi.

## 3. Sheria ya Makosa ya Mtandaoni na Sheria ya Takwimu zifanyiwe mabadiliko:

Kufuatia changamto zilizoonekana kwenye Sheria ya Makosa ya Mtandaoni tunashauri kwamba sheria hii ifanyiwe mabadiliko. Kama Sheria mpya inayoohusiana na Uhuru wa Kujieleza itatungwa, basi sheria hii ichukue vifungu chanya vya Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ambavyo vinajikita katika kusimamia shughuli zinazofanywa mtandaoni, kukiwa na sehemu maalumu kwa ajili ya makosa yanayoweza kufanyika.
Kama ilivyoelezwa awali, kuna mambo pia ya kujiangaliza kwenye Sheria ya Takwimu ambayo yanatakiwa yafanyiwe marekebisho. Bunge na Tume ya Kurekebisha Sheria zinatakiwa kuweka msisitizo katika kupitia sheria hizi ili kutoa ufafanuzi zaidi juu ya utata unaowekwa na sheria mbalimbali.

### 4. Kuweka kifungu cha ulinzi na kulinda uhuru wa kujieleza kwa asasi na wanachama wao:

Tunashauri Bunge kupitia Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria kuweka vifungu vitakavyotoa tasfiri ya 'maslahi ya umma' kwa sababu vifungu hivi vimekuwa vinatumika kuzuia Uhuru wa Kujieleza. Kifungu hiki kinaweza kuwekwa kama kifungu kipya kwenye sheria mpya zinazolinda Uhuru wa Kujieleza.

### 5. Itungwe sheria ambayo itaanzisha chombo huru cha usimamizi kwa ajili ya kutoa maamuzi juu ya weledi na maadili ya vyombo vya habari:

Ujumbe wetu kwa Serikali na Bunge ni kutoa msaada kwenye jitihada za wadau wa habari ili kuanzisha chombo cha kusimamia habari. Hii ni kwa ajili ya kukuza weledi wa sekta ya habari kwa ujumla, ambayo itakuwa na uwezo wa kupunguza maoni hasi juu ya maudhui ya vyombo vya habari. Hii inaweza kuboresha muonekano wa jamii juu ya vyombo vya habari. Bado ni muhimu pia kuwa nguvu za chombo hiki cha usimamizi zinabaki mikononi mwa wadau wa habari wenyewe ili kupunguza chombo hiki kutumika kisiasa.

### 6. Kuongeza uwekezaji ili kupata habari zilizoboreshwa ambazo zinapatikana kwa jamii nzima:

Kwa taifa lolote la kidemokrasia, uhuru wa kujieleza ni muhimu kwa ajili ya maendeleo. Taarifa zinatumika kama kiungo kati ya jamii na dola. Tunahitaji taarifa sahihi na zinazotoka kwa wakati. Tunaisisitiza serikali kuongeza juhudi za kuhakikisha kuwa taarifa za jamii zinakuwepo, zinaboreshwa na zinapatikana kwa ajili ya wanajamii.

Agosti 2016

Facilitated by UHAKIKI Project; a project funded with UK aid from the UK government

LHRC is a non-governmental organisation with core funding from the Royal Norwegian Embassy and the Embassy of Sweden